
TaCRI

TANZANIA COFFEE RESEARCH INSTITUTE

# DHIBITI KIDOMOZI KWA MAVUNO MENGI NA BORA YA KAHAWA



**Viwavi wa Kidomozi**



**Nondo wa Kidomozi**

# KIDOMOZI NI NINI

Kidomozi ni nondo mdogo mweupe ambaye mchana hujificha chini ya majani ya kahawa na kuruka usiku. Kidomozi hushambulia zaidi majani ya kahawa ya aina ya Arabika. Mashambulizi yanayofanywa na wadudu hawa hupunguza mazao kwa asilimia 8-10. Nondo wa kidomozi hutaga mayai juu ya majani ya kahawa na huangua viwavi wadogo ambao huharibu majani kwa kuacha makovu ya kahawia

**Dalili zake:**

- Majani yaliyoshambuliwa yanakuwa na mabaka ya rangi ya kahawia na juu ya jani linaonekana lina mabaka ya ukavu.

- Endapo ukifumua kovu kwa kutumia waya mwembamba utaona viwavi wadogo na weupe

**Madhara yake:**

- Mashambulizi ya viwavi hawa hupunguza eneo la majani linalotengeneza chakula cha mmea na kusababisha majani kupukutika

- Kupukutisha majani husababisha mti wa kahawa kushindwa kutengeneza chakula cha kutosha kujilisha na hasa kulisha matunda



*Mabaka kwenye jani la kahawa yaliyosababishwa na viwavi wa kidomozi*

## UDHIBITI

- Zingatia usafi wa shamba (kukata matawi, kukatua shamba na kuweka matandazo).
- Punguza kivuli shambani ili mwanga wa jua upenye kwa asilimia 60.
- Tumia viuatlifu vya asili kama mkojo wa ng'ombe kwa uwiano wa 1:4 (mkojo : maji) kwa kunyunyizia kwenye shamba la kahawa
- Tumia viuatilifu kama vile Chlopyrifos (Dursban) 48%EC mls 30/lita 15 za maji. Cypermethrin 51.5% EC .mls 20/lita 20 za maji.

**Angalizo:** Viuatilifu hivi vitumike wakati nondo 35 au zaidi wanapoonekana wakati mti wa kahawa ukitikiswa . Pia viuatilifu hivi vitumike wakati hatua ya viwavi wa mdudu huyu wakiwa wachache kwenye hatua ya kifukofuko (cocoon stage) .



**Hatua ya viwavi wakiwa kwenye kifukofuko (cocoon stage)**

## Mambo ya kuzingatia

- Tumia viuatilifu hivi baada ya wiki moja nondo wa mdudu huyu wanapokuwa wengi. Rudia tena kunyunyizia viuatilifu baada ya wiki 2 hadi 3.

- Badilisha viuatilifu vya kudhibiti mara kwa mara kwani utumiaji wa aina moja ya viuatilifu husababisha wadudu hawa kuwa sugu.

## Faida ya kudhibiti

- Atakuwa amepunguza kuzaliana kwa wadudu hawa.

- Atakuwa ameongeza wingi wa mavuno na ubora wa kahawa.

- Atakuwa amejiongezea kipato chake na kuwa na maisha bora zaidi

- Atakuwa ameongeza pato la taifa kwa ujumla

**Kimechapishwa na kusambazwa na:**
Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania (TaCRI)
S.L.P. 3004, Moshi, Tanzania
Simu:+255-27-2756868
Nukushi: +255-27-2756773
Barua Pepe: info@tacri.org
Tovuti: www.tacri.or.tz




TOLEO LA PILI JULAI 2018

©TaCRI 2018